

## **Ujitokezaji na Dhima za Yambwa katika Muundo wa Utendea wa Kimatengo na Kiswahili**

*Fokas Nchimbi<sup>1</sup>*

### **Ikisiri**

Miundo mbalimbali ya vitenzi vya lugha za Kibantu huweza kuamua ruwaza za utokeaji na dhima za kisemantiki za nomino za yambwa. Makala hii inachunguza mazingira ya utokeaji wa nomino za yambwa na dhima zake za kisemantiki katika lugha za Kimatengo na Kiswahili katika muundo wa kati wa utendea. Kufikia malengo hayo, makala hii inaongozwa na Nadharia ya Sarufi ya Uamilifu wa Kileksika inayomakinikia miundo miwili ya kisintaksia, yaani muundo wa kisintaksia unaowasilisha mfuatano wa maneno na makundi ya virai. Pili, muundo wa kisintaksia unaowasilisha uamilifu wa kisintaksia, kama vile kiima na yambwa. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa njia kuu mbili. Data zinazohusu lugha ya Kimatengo zilipatikana uwandani kwa kuwatumia wazungumzaji asilia wa lugha hiyo. Data za Kiswahili zilikusanywa kutoka katika matini mbalimbali. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwapo kwa aina mbili za yambwa katika muundo wa utendea katika Kimatengo na Kiswahili, yaani yambwa tendewa na yambwa tendwa. Yambwa hizo zinazojitokeza baada ya kitenzi tendea zina dhima mbalimbali za kisemantiki ambazo ni unufaika, uathirika, uelekeo, kifaa na sababu.

### **1.0 Utangulizi**

Kimatengo na Kiswahili ni lugha za Kibantu zinazozungumzwa katika eneo la Afrika Mashariki. Katika mgawanyo wa Guthrie wa lugha za Kibantu, lugha ya Kimatengo imewekwa kwenye kundi N 13. Wazungumzaji wa Kimatengo wapatao 470,000 wanaishi katika eneo la milima la Kusini Magharibi mwa Tanzania katika maeneo ya kiutawala ya wilaya ya Mbinga na katika baadhi ya maeneo ya kiutawala ya wilaya ya Nyasa (Mbele, 1999; Nchimbi, 2004).

Kwa mujibu wa mgawanyo wa lugha za Kibantu uliofanywa na Guthrie, lugha ya Kiswahili imewekwa kwenye kundi G 42. Katika nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kiswahili ni lugha ya taifa na lugha rasmi ya mawasiliano ya kitaifa (Roy-Campbell na Qorro, 1997). Aidha, lugha ya Kiswahili imeenea na kuzungumzwa katika nchi nyingi za Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, na nchi nyingine katika bara la Afrika kama

---

<sup>1</sup> Mhadhiri, Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Iringa, Tanzania. Barua pepe: fokanchimbi@gmail.com

vile Misri, Libya, Ghana na Naijeria (Mtesigwa, 2023). Kwa mujibu wa Mtesigwa (*keshatajwa*), lugha ya Kiswahili imeshaenea kwenye nchi za bara la Ulaya, Asia na Amerika. Miongoni mwa mataifa ambako lugha ya Kiswahili inazungumzwa barani Ulaya ni Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Italia, Denmaki, Ufini, Norwei, Hispania, Urusi, Uholanzi na Hungaria. Barani Asia, lugha ya Kiswahili inazungumzwa Uchina, Ujapani, Korea, India, Saudi Arabia, Omani na Muscat. Katika bara la Amerika, lugha ya Kiswahili inazungumzwa katika nchi za Marekani, Kanada, Kyuba, Meksiko, Brazili na Jamaika. Kwa mujibu wa Mtesigwa (*keshatajwa*), kuongezeka kwa wazungumzaji wa Kiswahili duniani ni sababu mojawapo iliyolifanya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), mnamo tarehe 23/11/2021, kutangaza rasmi tarehe 7 mwezi wa 7 kila mwaka kuwa siku rasmi ya kuadhimisha lugha ya Kiswahili duniani kote.

Lugha za Kimatengo na Kiswahili zinasibishwa na lugha nyingine za Kibantu kwa sababu ya kuwa na sifa zinazofanana kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki. Ufafanuzi wa mofolojia ya vitenzi katika lugha za Kibantu unaonesha kuwa kuna aina mbalimbali za miundo ya vitenzi inayoathiri hali ya uelekezi wa vitenzi katika lugha hizo (Kapinga, 1983; Habwe na Karanja, 2004; Kihore na wenzake, 2008; Massamba na wenzake, 2009; Matinde, 2012). Uelekezi wa kitenzi ni uwezo wa kitenzi kuhitaji kujalizwa kwa nomino ya yambwa kwenye muundo wa sentensi. Uwezo wa kitenzi kuhitaji kujalizwa kwa nomino ya yambwa unatokana na maana ya kitenzi inayoonesha kuwa kitendo kinaelekezwa kwenye kishiriki cha sentensi ambacho ni nomino ya yambwa.

Kwa kutumia mkabala huo wa uelekezi katika vitenzi vya lugha za Kibantu, kuna vitenzi elekezi na vitenzi ambavyo si-elekezi. Vitenzi elekezi ni vile ambavyo vinapotumika kwenye muundo wa sentensi vinahitaji kukamilishwa na yambwa. Vitenzi si-elekezi ni vile ambavyo vinapotumika kwenye muundo wa sentensi havihitaji kukamilishwa na yambwa (Kihore, 2009).

Kuna ufafanuzi wa aina mbalimbali kuhusu yambwa katika lugha za binadamu, zikijumuishwa lugha za Kibantu, ambapo kuna mwelekeo wa kutambua na kutaja aina mbili za yambwa: yambwa tendewa na yambwa tendwa. Hivyo, makala hii inatambua kuwapo kwa yambwa tendewa na yambwa tendwa. Makala hii imelenga kuchunguza utokeaji wa nomino za yambwa tendewa na yambwa tendwa katika muundo wa utendea katika Kimatengo na Kiswahili. Pili, makala inachunguza dhima za kisintaksia na kisemantiki za aina hizo za yambwa katika muundo wa utendea wa lugha hizo mbili.

Ufafanuzi wa mofolojia ya vitenzi katika lugha za Kibantu unaonesha kuwa kuna aina mbalimbali za miundo ya vitenzi (Kapinga, 1983; Habwe na Karanja, 2004; Kihore na wenzake, 2008; Massamba na wenzake, 2009; Matinde, 2012). Kwa upande mmoja, kwa kutumia kigezo cha valensi na uelekezi wa vitenzi vya lugha za Kibantu, kuna vitenzi elekezi na vitenzi ambavyo si elekezi. Kwa ujumla, kwa kutumia kigezo cha mofolojia ya vitenzi vya lugha za Kibantu,

kuna miundo tenda, kati na tendwa. Miundo tenda inatokana na miundo asilia ya vitenzi ambavyo vinatumika bila kufanyiwa unyambuzi (Rubanza, 2003). Miundo kati ni miundo yote inayotokana na michakato ya kimofolojia ya unyambuzi. Kwa maneno mengine, hiyo ni miundo yote ambayo si miundo tenda na wala tendwa.

## **2.0 Mapitio ya Maandiko**

Sehemu hii inawasilisha kwa ufupi mapitio ya maandiko mbalimbali kuhusu muundo nyambuzi wa utendea katika lugha za Kibantu. Ufafanuzi kuhusu muundo wa utendea katika lugha za Kibantu unahusisha mazingira ya utokeaji wa nomino za yambwa pamoja na dhima zake kisintaksia na kisemantiki.

### **2.1 Muundo wa Utendea**

Kuna maandiko mengi yanayofafanua dhana ya miundo ya vitenzi katika lugha za Kibantu (Khamis, 2008; Tallerman, 2011; Matinde, 2012). Mazingira ya utokeaji na dhima za nomino za yambwa huamuliwa na aina ya muundo wa kitenzi, maana ya kitenzi na maana ya nomino husika ya yambwa. Utendea ni mojawapo ya aina za miundo zalishi ya vitenzi katika lugha mbalimbali duniani ikiwa ni pamoja na lugha za Kibantu. Matinde (2012) anatoa ufafanuzi kuhusu maana ya dhana ya muundo wa utendea kwa kusema kuwa muundo huo unahusisha uhusiano wa ‘kwa niaba ya’ au ‘kwa manufaa ya’ baina ya kiima na yambwa. Hii ina maana kwamba muundo huo unaonesha kuwa nomino iliyopo sehemu ya kiima katika muundo wa ndani wa uhusika inatenda kwa niaba au kwa ajili ya manufaa ya nomino inayojitokeza katika sehemu ya kiarifu kama yambwa.

Tallerman (2011) anafafanua kuwa utendea ni muundo wa kati wa vitenzi katika lugha za Kibantu unaozaa nomino mbili za yambwa, yaani yambwa tendewa na tendwa. Anafafanua kuwa miundo ya utendea inatokana na miundo ya msingi ya utenda kwa kutumia mchakato wa ukwezwaji na ushushwaji wa vikundi vihusishi na vikundi nomino. Khamis (2008) anatumia neno mufidi akirejelea dhana ya muundo kati wa kitenzi wa utendea. Katika maelezo yake anafafanua kuwa wakati ambapo Kiingereza hutumia vihusishi kuwasilisha muundo wa utendea, katika Kiswahili kuna uhuru wa kuwasilisha muundo huo kwa kukinyambulisha kitenzi kutoka muundo asilia tenda hadi kuwa katika muundo nyambuo wa utendea.

### **2.2 Dhana ya Yambwa na Dhima zake**

Hakuna fasili moja na ya moja kwa moja ya dhana ya yambwa. Wanasarufi mbalimbali wanafafanua kwamba yambwa ni sehemu ya tungo inayorejelea kitu au mtu anayelengwa na kitendo kinachotekelezwa (Robins, 1965; Freeborn, 1995; Kiango, 2000; Massamba, 2004; Asumpta na Matei, 2008). Wanasarufi wengine wanafasili dhana ya yambwa kuwa ni elementi au kipashio cha kiarifu ambacho hueleza kuhusu manufaa au athari ya kitendo (Besha, 1994; Barwani, 1995; Mgullu, 1999; Radford, 2009; Habwe na Karanja, 2014). Fasili hizo za yambwa

zimekitwa hasa kwenye dhana ya dhima mbili za kisemantiki za yambwa, yaani dhima ya kisemantiki ya unufaika na ya kisemantiki ya uathirika. Fasili katika maandiko hayo hazioneshi sababu inayoamua aina ya dhima za kisemantiki zinazoweza kubainishwa kwenye nomino ya yambwa.

Maandiko mengine yanafanua dhana ya yambwa kwa kueleza kuwa kipashio ambacho ni kitendwa au kitendewa cha kitendo (Yule, 1985; Schadeberg, 1996; Jerono, 2003). Maandiko hayo yanajikita kwenye aina mbili za yambwa ambazo ni yambwa tendewa na tendwa. Maandiko hayo hayafanui dhima za yambwa wala sababu inayoweza kuamua aina ya dhima za kisemantiki zinazoweza kubainishwa kwenye nomino ya yambwa tendewa au tendwa.

Aidha, Hyman na Duranti (1982) wanatoa ufafanuzi wa dhana ya yambwa kwa kuorodhesha vigezo vikuu vitatu vinavyoweza kutumika kuibainisha yambwa katika lugha za Kibantu. Vigezo hivyo vya utambuzi wa yambwa katika lugha za Kibantu ni mfuatano wa maneno, ukiima na uyambishaji katika kitenzi elekezi. Kigezo cha kwanza kinahusu dhana kwamba yambwa katika lugha za Kibantu inafuata baada ya kitenzi elekezi. Kigezo cha pili kinahusu uwezo wa yambwa kuwa kiima cha muundo tendwa na kigezo cha tatu kinahusu uwakilishwaji wa kiambishi cha yambwa kwenye kitenzi elekezi cha lugha za Kibantu.

Tofauti kidogo na fasili ya Hyman na Duranti, kuna ufafanuzi wa dhana ya yambwa unaotolewa na Rugemarila (1993) na Schalderbeg (1995). Rugemarila na Schalderbeg wanaorodhesha vipimio vitatu vya yambwa vinavyotumiwa na Bresnan na Moshi (1993) kuelezea upacha na usopacha wa lugha za Kibantu kuhusiana na sifa za yambwa katika lugha za Kibantu. Vipimio hivyo ni mfuatano wa maneno, upatanishi wa kisarafu na ukiima wa nomino ya yambwa. Ujitokezaji wa nomino za yambwa katika lugha mbalimbali, ikiwa ni pamoja na lugha za Kibantu, huamuliwa na maana msingi ya muundo wa kitenzi na maana ya nomino husika ya yambwa. Miundo muhimu nyambuzi ya vitenzi katika Kiswahili ni utenda, utendesha, utendeshea, utendea, utendano, utendeano, utendeka, utendesheano, utendua, ujirejea na utendwa (Matinde, 2012). Tofauti na Kiswahili, katika lugha ya Kimatengo hakuna muundo wa utendwa.

Miongoni mwa miundo iliyoorodheshwa hapo juu, kuna miundo inayoamua kutotokea kabisa kwa nomino za yambwa. Kwa kawaida, hiyo ni miundo tenda ambayo si-elekezi katika Kimatengo na Kiswahili. Pia, miundo mwingine unaoamua kutotokea kwa yambwa ni muundo wa utendeka. Miundo mingine ya vitenzi vya lugha za Kibantu inasababisha kupungua kwa idadi ya yambwa katika sentensi za Kimatengo na Kiswahili. Miundo inayopunguza idadi ya yambwa katika sentensi za Kimatengo na Kiswahili ni miundo ya utendano, utendeano na utendesheano.

Aidha, kuna miundo inayoamua kudumisha idadi ileile ya nomino za yambwa katika sentensi za Kimatengo na Kiswahili. Miundo hiyo katika lugha ya Kiswahili inajumuisha utendua, ujirejea na utendwa. Katika lugha ya Kimatengo, miundo inayoamua kudumisha idadi ileile ya nomino za yambwa katika sentensi ni

utendua na ujirejea. Halikadhalika, kuna miundo inayoamua kuongezeka kwa idadi ya yambwa katika sentensi za Kimatengo na Kiswahili. Miundo hiyo inajumuisha utenda elekezi, utendesha, utendeshea na utendea.

### 3.0 Mbinu za Utafiti

Data zilizotumika kuandika makala hii zimekusanywa uwandani kwenye vijiji vitatu vya wilaya ya Mbinga, Kusini Magharibi mwa Tanzania. Vijiji hivyo ni Myangayanga, Kindimba na Wukiro. Vijiji hivyo vipo katika eneo la Umatengo ambapo wazungumzaji wazawa wa Kimatengo walisampulishwa kwa mbinu ya usampulishaji kusudio. Wazee watatu wa Kimatengo walichaguliwa na kuombwa kumsaidia mtafiti kuwabainisha watu wengine 17 wanaoweza kuzungumza Kimatengo kama lugha yao mama. Kwa ujumla, wahojiwa katika utafiti huu walikuwa wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kimatengo ambao hawajapata athari kubwa ya lugha nyingine hasa Kiswahili. Katika uchunguzi huu kulikuwa na jumla ya wahojiwa 20; wanawake 10 na wanaume 10. Data zilizokusanywa kwa njia ya hojaji zilihakikiwa kwa njia ya mahojiano yaliyofanywa baina ya mtafiti na wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kimatengo.

Data zilikusanywa kwa kutumia hojaji na mahajiano ambapo lengo lilikuwa kubainisha sentensi zenye vitenzi vya miundo ya utendea ya Kimatengo yenye kuwasilisha dhima mbalimbali za kisemantiki za nomino za yambwa. Data za Kiswahili zilikusanywa kutoka kwenye vitabu vya sarufi maumbo na sarufi miundo ya Kiswahili pamoja na *Biblia*. Vyanzo hivyo vya data za lugha ya Kiswahili vilichaguliwa kwa sababu lugha ya Kiswahili ina maandiko mengi ya kisarufi na mengineyo kuliko ilivyo katika lugha ya Kimatengo. Uchunguzi katika matini hizo ulilenga kubainisha miundo ya utendea ya Kiswahili na kuchunguza dhima za kisemantiki zinazotokana na miundo hiyo ya utendea. Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Sarufi ya Uamilifu wa Kileksika ambayo ni mkabala unaoangalia uamilifu wa kisintaksia na kisemantiki wa kiima na yambwa kama viambajengo msingi na majumui katika mfumo wa kisarufi wa lugha za wanadamu. Waasisi wa Nadharia hii ni wanaisimu Joan Bresnan na Ronald Kaplan mwishoni mwa miaka ya 1970.

Nadharia ya Sarufi ya Uamilifu wa Kileksika inaunganisha kategoria ya kileksika ya yambwa na dhima zake za kisintaksia na kisemantiki katika miundo ya sentensi inayoamuliwa na maumbo mbalimbali ya vitenzi (Johnson, 2004; Lusekelo, 2013). Misingi ya Nadharia ya Sarufi ya Uamilifu wa Kileksika inaeleza kwamba katika lugha kuna miundo miwili ya uambajengo. Muundo wa kwanza ni uambajengo unaowasilisha mfuatano wa maneno na makundi ya virai. Muundo wa pili ni uambajengo unaowasilisha uamilifu wa kisintaksia wa kiima na yambwa. Katika makala hii, Nadharia ya Sarufi ya Uamilifu wa Kileksika imetumika katika uchambuzi wa ushiriki wa ndani unaotokana na muundo wa kitenzi wa utendea kwa kuangazia uhusiano baina ya muundo wa uambajengo na muundo wa uamilifu. Msingi wa kwanza wa muundo wa uambajengo umetumika kuchambua

na kuwasilisha muundo wa vitenzi vya utendea na mfuatano wake wa kiuhusiano na nomino za yambwa. Imeoneshwa kuwa muundo wa utendea wa kitenzi katika Kimatengo na Kiswahili huhitaji kukamilishwa na kijalizo yambwa. Msingi wa pili ni muundo wa uamilifu ambao umetumika kuchambua dhima za yambwa kisemantiki zinazotokana na muundo wa kitenzi wa utendea na mfuatano wa kiuhusiano na nomino za yambwa. Msingi huo umeonesha kuwa maana ya vitenzi na nomino za yambwa huamua aina ya dhima za kisemantiki za yambwa husika. Uwasilishaji wa data katika makala hii umegawika katika makundi mawili. Kundi la kwanza la uwasilishaji wa data linahusu data za lugha ya Kimatengo. Kundi la pili linahusu uwasilishaji wa data za lugha ya Kiswahili.

#### 4.0 Yambwa katika Miundo ya Utendea

Katika Kimatengo umbo la utendea linaweza kuvifanya vitenzi si elekezi kuwa vitenzi elekezi na hivyo kubadilisha muundo wa ushiriki kutoka ushiriki wa nomino moja hadi ushiriki wa nomino mbili. Ushiriki wa nomino mbili una nomino moja ya yambwa tendewa inayotokana na umbo la utendea katika Kimatengo. Kwa mfano:

1. (a) Mwana jualelila anyongo bake.  
*Mtoto alimlilia mama yake.*
- (b) Mwenei juang'anambukia ageni.  
*Mwenyeji aliwageukia wageni.*
- (c) Mundu juatamila kiteu.  
*Mtu alikalia kiti.*
- (d) Yesu anzendila mbomba jola  
*Yesu alimwendea yule mwanamke.*

#### **Chanzo: Data za Uwandani (2023)**

Data ya 1(a), (b), (c) na (d) zinaonesha kuwa vitenzi vyake vyote, yaani 'lela' (lia), 'ng'anambuka' (geuka), 'tama' (kaa), na 'jenda' (nenda) ni maumbo si elekezi katika miundo yake ya msingi. Kutokana na kukosa sifa ya uelekezi, vitenzi hivyo havihitaji kukamilishwa na yambwa. Aidha, vinapoingia katika maumbo ya utendea, vitenzi hivyo hivyo vinakuwa na sifa ya uelekezi unaoviwezesha kuwa na yambwa tendewa moja. Kutokana na uelekezi unaosababishwa na unyambuzi tendea wa vitenzi husika, kuna uibuzi wa maumbo nyambuzi 'jualelila anyongo' (alimlilia mamaye), 'juang'anambukia ageni' (aliwageukia wageni), 'juatamila kiteu' (alikalia kiti), na 'anzendila mbomba jola' (alimwendea yule mwanamke). Yambwa tendewa 'anyongo' (mama), 'ageni' (wageni), 'kiteu' (kiti) na 'mbomba' (mwanamke) katika Data 1(a), (b), (c) na (d) zinatokea mara baada ya vitenzi husika.

Halikadhalika, katika Kiswahili, kuna vitenzi si elekezi ambavyo kwa asili vinaweza kuambishwa mofu ya umbo la utendea, na hivyo, kufuatiwa na yambwa tendewa moja.

Kwa mfano:

2. (a) Akamgeukia (yule) mwanamke.
- (b) Walioko makaburini wataisikia sauti yake.
- (c) Mafarisayo wakamkusanyikia Pilato.
- (d) Mtu huyu alimwendea Pilato.

**Chanzo: Biblia (2004)**

Data ya 2(a), (b), (c) na (d) zinawasilisha vitenzi ‘akamgeukia’, ‘wataisikia’, ‘wakamkusanyikia’ na ‘alimwendea’ mtawalia, ambavyo kwa asili vina maumbo tenda si-elekezi. Baada ya kuambikwa mofu ya utendea {-i-} katika 2(a), (b) na (c); na mofu ya utendea {-e-} katika 2(d), vitenzi hivyo vinakuwa elekezi na kuwa na uwezo wa kubadilisha muundo wa ushiriki kutoka muundo wa kishiriki kimoja hadi kuwa na muundo wa ushiriki wa vishiriki viwili. Muundo wa ndani wa ushiriki huo unaundwa na nomino za yambwa tendewa ‘mwanamke’, ‘sauti’, ‘Pilato’ na ‘Pilato’ kwa kila sentensi, mtawalia. Kwa hiyo, kulingana na Data ya 1(a), (b), (c) na (d) na 2(a), (b), (c) na (d) inaoneshwa kuwa mazingira ya utokeaji wa yambwa tendewa katika umbo la utendea yanafanana katika Kimatengo na Kiswahili.

Aidha, umbo la utendea linasababisha uelekezi wa yambwa mbili katika Kimatengo na Kiswahili. Uwezekano huo hutokana na maana ya msingi ya vitenzi ambapo ili kubadilishwa na kuwa na maumbo ya utendea, sharti viwe na uelekezi wa yambwa mbili. Katika Kimatengo kuna vitenzi vichache vinavyoweza kuchukua umbo la utendea lenye uelekezi wa yambwa mbili.

Kwa mfano:

3. (a) Ndemi juatekila abengi masi  
*Mkulima aliwachotea wawindaji maji.*
- (b) Amabu baahogulia bana itabo  
*Mama aliwafungulia watoto vitabu.*
- (c) Ndemi ampulila ndimi kipungu  
*Mkulima alimpulizia mfungaji upupu.*
- (d) Ndepi juaholela atate kujomoka  
*Mlevi alimzushia baba kufa.*

**Chanzo: Data za Uwandani (2023)**

Katika Data ya 3(a), (b), (c) na (d) nomino za yambwa tendewa ‘abengi’ (wawindaji), ‘bana’ (watoto), ‘ndimi’ (mfugaji), na ‘atate’ (baba) mtawalia, zinatokea mara baada ya vitenzi vya Kimatengo ‘juatekila’ (aliwachotea),

‘hogulia’ (aliwafungulia), ‘ampulila’ (alimpulizia) na ‘juaholila’ (alimzushia), mtawalia. Huu ni mfuatano wa kawaida wa yambwa mbili katika sentensi ya Kimatengo inayotokana na umbo la utendea. Hata hivyo, mazingira hayo ya utokeaji wa yambwa tendewa na yambwa tendwa katika utendea yanaweza kubadilika ikiwa msemaji anaonesha msisitizo kwenye yambwa tendwa. Katika mazingira hayo, yambwa tendwa inaweza kukwezwa na kutokea mara baada ya kitenzi na hivyo kufuatiwa na yambwa tendewa.

Kwa mfano:

4. (a) Ndemi antekila masi mbengi  
*Mkulima alimchotea maji mwindaji.*
- (b) Amabu bahogolia itabu bana  
*Mama aliwafungulia vitabu watoto.*
- (c) Ndemi juapulisia kipungu alimi  
*Mkulima aliwapulizia upupu wafugaji.*
- (d) Ndepi juaholila kujomoka atati  
*Mlevi alimzushia kifo baba.*

#### **Chanzo: Data za Uwandani (2023)**

Data ya 4(a), (b), (c) na (d) zinaonesha kuwa kuna mabadiliko kuhusiana na mfuatano wa yambwa tendewa na tendwa. Katika data hizo, yambwa tendwa ‘masi’ (maji), ‘itabo’ (vitabu), ‘kipungu’ (upupu) na ‘kujomoka’ (kufa) zimefuata mara baada ya kitenzi na kufuatwa na nomino za yambwa tendewa ‘mbengi’ (mwindaji), ‘bana’ (watoto), ‘alimi’ (wafugaji) na ‘atate’ (baba) mtawalia. Sintaksia ya Kimatengo inaruhusu usarufi wa mfuatano wa nomino za yambwa unaowakilishwa na Data ya 4(a), (b), (c) na (d) kwa ajili ya kuonesha msisitizo kwenye kipashio husika. Pamoja na usarufi wa mfuatano huo, mfuatano uliowakilishwa katika Data ya 3(a), (b), (c) na (d) ndio mfuatano wa kawaida katika sintaksia ya Kimatengo.

Umbo la utendea katika Kiswahili linaweza kuvifanya vitenzi si elekezi kuwa vitenzi elekezi, hivyo, kuathiri muundo wa ushiriki kutoka ushiriki wa nomino moja hadi ushiriki wa nomino mbili. Ushiriki wa nomino mbili unaruhusu kitenzi kuwa na yambwa tendwa moja.

Kwa mfano:

5. (a) Mama alimkimbilia mtoto wake (Mohamed, 1986).
- (b) Farao aliwakasirikia watumwa wake (*Biblia*, 2004).

Data ya 5(a) na (b) zinaonesha kuwa vitenzi vyote, yaani ‘alimkimbilia’ na ‘aliwakasirikia’ si maumbo elekezi kwa asili yake, yaani katika maumbo yake ya msingi. Katika maumbo ya utendea, shina la kitenzi likiwa na irabu ‘aa’, ‘ia’ au ‘ua’ kitenzi huambikwa kiambishi ‘-li-’ Vitenzi hivyo katika Data ya 5(a) na (b) vinaacha maswali ambayo yanahitaji kujibiwa kwa kuwapo kwa nomino moja ya



yambwa tendwa. Maswali hayo ni: ‘Mama alimkimbilia nani?’ ‘Farao aliwakasirikia akina nani?’ Nomino ‘mtoto’ na ‘watumwa’ katika Data ya 5(a) na (b) za yambwa tendewa zinatokea mara baada ya vitenzi husika ili kujibu maswali hayo.

Aidha, umbo la utendea linaweza kuamua uelekezi wa yambwa mbili. Katika Kiswahili na Kimatengo, uwezekanao huo hutokana na maana ya msingi ya vitenzi ambavyo kama vikibadilishwa maumbo yake huwa na maumbo ya utendea yenye uelekezi wa yambwa mbili. Katika Kiswahili kuna vitenzi ambavyo vina uwezo wa kuchukua maumbo ya utendea yenye uelekezi wa yambwa mbili.

Kwa mfano:

6. (a) Musa anamwandikia Jeni barua.
- (b) Jesse anampikia baba ugali.
- (c) Stacy alimwandikia mpenzi wake barua.

#### **Chanzo: Habwe na Karanja (2004)**

Data ya 6(a), (b) na (c) zinaonesha maumbo ya utendea yenye uelekezi wa yambwa tendewa na yambwa tendwa katika ‘anamwandikia’, ‘anampikia’ na ‘alimwandikia’, mtawalia. Katika umbo hili la yambwa mbili, yambwa tendwa na yambwa tendewa kwa pamoja zinazuia maswali ambayo awali katika Data ya 6(a), (b) na (c) yaliweza kuulizwa katika mazingira ya utokeaji wa yambwa moja tu. Katika mazingira ya utokeaji wa yambwa mbili, yambwa tendwa hufanya ukamilishaji wa kitenzi husika, na hivyo kuzuia mwanya wa kuulizwa kwa maswali.

#### **5.0 Dhima za Yambwa katika Utendea**

Sehemu hii inawasilisha na kuchambua data zinazoonesha matumizi ya yambwa tendewa na tendwa kisintaksia na kisemantiki katika umbo la utendea. Kwa mujibu wa Nadharia ya Sarufi ya Uamilifu wa Kileksika, hii ni ngazi ya pili ya uwasilishaji wa viambajengo vya tungo katika lugha.

#### **5.1 Dhima za Kisintaksia za Yambwa katika Utendea**

Katika Kimatengo, yambwa tendwa kwenye umbo la utendea la yambwa moja inafanya kazi ya kisintaksia ya kuwa yambwa tendwa. Katika umbo la ushiriki la ndani la nomino moja, nomino haina budi kufuata mara baada ya kitenzi cha sentensi kama yambwa tendwa inayokikamilisha au kukijaliza kitenzi elekezi cha umbo la utendea.

Kwa mfano:

7. (a) Ambuja ambutukia mwana  
*Bibi alimkimbilia mtoto.*
- (b) Mbomba juaholila bana bake  
*Mwanamke aliwahofia watoto wake.*

- (c) Ndepi juikanyatia ibana  
*Mlevi alivikanyaga vifaranga.*
- (d) Mwana juahyomila akahengo bake  
*Mtoto aliwakasirikia wazazi wake.*

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Katika Data ya 7(a), (b), (c) na (d), maumbo ya utendea katika kila sentensi yanatokana na maumbo ya vitenzi si elekezi ‘butuka’ (kimbia), ‘hola’ (hofu), ‘kanyata’ (kanyaga) na ‘hyoma’ (sikitika). Nomino ‘mwana’ (mtoto), ‘bana’ (watoto), ‘ibana’ (vifaranga) na ‘akahengo’ (wazazi) zinazofuata baada ya vitenzi husika ni yambwa tendwa zinazofanya kazi ya kuvikamilisha vitenzi nyambuo elekezi vya umbo la utendea wa yambwa moja.

Kwenye umbo la utendea lenye uelekezi wa yambwa mbili, data za utafiti huu zinabainisha kuwa umbo hilo lina yambwa tendewa na yambwa tendwa. Katika mazingira ya utokeaji wa pamoja wa aina hizo za yambwa, yambwa tendewa kwa kawaida, hutokea mara baada ya kitenzi na kufuatiwa na yambwa tendwa. Yambwa tendewa na tendwa zina dhima ya kutekeleza kisintaksia. Uchambuzi na uwasilishaji wa data katika utafiti huu unabainisha kuwa yambwa tendewa ina dhima ya kisintaksia ya kukikamilisha kitenzi elekezi cha umbo la utendea. Pia, dhima ya kisintaksia ya yambwa tendwa katika umbo la utendea ni kukikamilisha kitenzi elekezi.

Kwa mfano:

8. (a) Amabo baasapila bana ingobu  
*Mama aliwafulia watoto nguo.*
- (b) Mwenei juakamulia ageni ingoku  
*Mwenyeji aliwakamatia wageni kuku.*
- (c) Ndemi juijegelia imboku sumo  
*Mkulima aliwawekea panya sumu.*
- (d) Ndepi juajitilia akakamwale masi  
*Mlevi aliwamwagia wasichana maji.*

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Katika Data ya 8(a), (b), (c) na (d) nomino za yambwa tendwa ni ‘ingobu’ (nguo), ‘ingoku’ (kuku), ‘sumo’ (sumu), na ‘masi’ (maji), mtawalia. Nomino hizo za yambwa tendwa, hufanya kazi ya kisintaksia ya kuvikamilisha vitenzi elekezi ‘baasapila’, ‘juakamulia’, ‘juijegelia’ na ‘juajitia’ katika data hiyo. Ukamilishaji huo unajibu au unazuia maswali yafuatayo: ‘Mama aliwafulia watoto nini?’ ‘Mwenyeji aliwakamatia wageni nini?’ ‘Mkulima aliwawekea panya nini?’ ‘Mlevi aliwamwagia wasichana nini?’

Halikadhalika, katika Kiswahili yambwa tendwa inayotokana na umbo la utendea la yambwa moja inafanya kazi ya kisintaksia kama ilivyo katika Kimatengo, yaani kazi ya kuvikamilisha kitenzi elekezi cha yambwa mbili.

Nomino ya yambwa tendwa katika umbo nyambuzi elekezi la yambwa moja kwenye sentensi ya Kiswahili, hufuata mara baada ya kitenzi cha sentensi na kutekeleza dhima ya kukikamilisha kitenzi nyambuo elekezi cha umbo la utendea. Kwa mfano:

9. (a) Mafarisayo wakamkusanyikia Pilato.
- (b) Farao aliwakasirikia watumwa wake.

**Chanzo:** *Biblia* (2004)

Katika Data ya utafiti ya 9(a) na (b) vitenzi vya sentensi hizo ‘wakamkusanyikia’ na ‘aliwakasirikia’, mtawalia, hutokana na maumbo ya vitenzi ambavyo kwa asili yake si elekezi, yaani ‘kusanyika’ na ‘kasirika’. Katika maumbo ya utendea, vitenzi hivyo vinapata uwezo wa kuwa na uelekezi wa nomino moja ya yambwa tendewa ‘Pilato’ na ‘watumwa’ kama inavyowasilishwa kwenye Data ya 9(a) na (b) mtawalia.

Katika Kiswahili, si vitenzi vyote vina uwezo wa kuwa na yambwa katika muundo wa tungo, hasa tukijiegemeza katika vitenzi si-elekezi katika maumbo yake ya asili. Nomino za yambwa tendewa za Data ya 9(a) na (b), yaani ‘Pilato’ na ‘watumwa’ zimefuata baada ya vitenzi husika vya yambwa tendewa na kufanya kazi ya kuvikamilisha vitenzi nyambuzi elekezi katika maumbo ya utendea ya yambwa moja. Uwezo huo wa kuwa na yambwa hauwezi kujitokeza katika vitenzi hivyo katika maumbo yake ya asili.

Halikadhalika, kwenye umbo la utendea lenye uelekezi wa yambwa mbili, kuna yambwa tendewa na tendwa. Yambwa tendewa na tendwa zote hutokea kwa mfuatano huo baada ya kitenzi na zinakuwa na dhima ya kutekeleza kisintaksia, yaani ya kukikamilisha kitenzi elekezi kama inavyowasilishwa kwenye Data ya 10(a), (b) na (c).

Kwa mfano:

10. (a) Ali amewanunulia watoto nguo.
- (b) Juma amemlimia mzee wake shamba.
- (c) Juma amemtolea askari kitambulisho.

**Chanzo:** Mohamed (1986)

Data ya 10(a), (b) na (c) zinawasilisha nomino za yambwa tendewa ‘watoto’, ‘mzee’ na ‘askari’ mtawalia. Kisintaksia nomino hizo zina dhima ya kukikamilisha kitenzi elekezi cha umbo la utendea. Nomino za yambwa tendewa katika Data ya 10(a) na (b), ‘nguo’, ‘shamba’ na ‘kitambulisho’ mtawalia, katika umbo la utendea hufanya kazi ya kukamilisha vitenzi elekezi ‘amewanunulia’, ‘amemlimia’ na ‘amemtolea’. Nomino hizo za yambwa katika umbo la utendea, pamoja na kufanya kazi ya kuvikamilisha vitenzi elekezi husika kisintaksia, ukamilishaji huo huenda sanjari na kuzuia au kujibu maswali ambayo yangeweza kujitokeza katika mfuatano wa maneno katika tungo husika. Kutokana na maana ya msingi ya

vitenzi ‘amewanunulia’, ‘amemlimia’ na ‘amemtolea’, maswali yafuatayo yanguweza kuulizwa kama yambwa tendwa isingelikuwapo: ‘Ali amewanunulia watoto nini?’ ‘Juma amemlimia babu nini?’ ‘Juma amemtolea askari nini?’

## 5.2 Dhima za Kisemantiki za Yambwa katika Utendea

Sehemu hii inawasilisha na kujadili dhima za kisemantiki za nomino za yambwa kwenye umbo la utendea katika Kimatengo na Kiswahili. Dhima za kisemantiki ni kategoria zinazoonesha maana zinazobebwa na kuwasilishwa na maumbo ya kitenzi kwa uzingatizi wa uhusiano wake na nomino zinazoambatana nazo kwenye muundo wa sentensi. Katika muundo wa ushiriki wa ndani, vishiriki vya sentensi hushirikiana na kitenzi cha umbo la ushiriki kujenga maana. Hivyo, kuwasilisha dhima zake za kisemantiki.

Katika lugha za Kimatengo na Kiswahili, nomino za yambwa katika umbo la utendea, zinaweza kuwa na dhima nyingi za kisemantiki kutegemeana na maana ya msingi ya kitenzi husika na uhusiano wake na nomino husika ya yambwa. Katika utafiti huu, dhima kuu nne (4) zimebainishwa na kujadiliwa kulingana na data za utafiti zinazohusu umbo la utendea. Dhima hizo za kisemantiki za umbo la utendea zinajumuisha kuonesha unufaika wa kishiriki, uathirikaji wa kishiriki, mwelekeo wa kutoka au kwenda kwa kishiriki na kifaa cha utekelezaji wa tendo au kazi pamoja na sababu ya kitendo.

### 5.2.1 Dhima ya Unufaika katika Utendea

Unufaika katika taaluma ya isimu ni dhima ya kisemantiki inayoonesha kuwa mtu fulani au kikundi fulani cha watu, kitu au kundi fulani la vitu linanufaika na jambo lililotendwa, linalotendwa au litakalotendwa. Katika Kimatengo, yambwa inayotokana na umbo la utendea inadhihirisha dhima ya unufaikaji kutegemeana na maana msingi ya kitenzi na yambwa husika.

Kwa mfano:

11. (a) Mbengi juasekulia alemi inyama  
*Mwindaji alimkatia mkulima nyama.*
- (b) Ndemi juatekila abengi mase  
*Mwindaji aliwachotea wawindaji maji.*
- (c) Ndimi juatotulia alemi luhanzu  
*Mfugaji aliwachukulia wakulima kuni.*
- (d) Kipesa saanukulia anakapundu litoki  
*Sungura alimkatia mbweha ndizi.*

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Nomino za yambwa tendewa ‘ndemi’ (mkulima), ‘abengi’ (wawindaji), ‘alemi’ (wakulima) na ‘anakapundu’ (mbweha) katika Data ya 11(a), (b), (c) na (d) mtawalia, ni wanufaika wa vitendo vinavyotekelezwa na vishiriki vya nje kwa kutumia vitenzi ‘juasekulia’ (aliwakatia), ‘juatekila’ (aliwachotea), ‘juatotulia’

(aliwachukulia) na ‘saanukulia’ (alimkatia). Dhima hizo za yambwa za unufaika kwenye nomino hizo za yambwa tendewa zinaamuliwa na maana ya msingi ya vitenzi na uhusiano wake na vishiriki vya ndani vya nomino za yambwa tendewa na nomino za yambwa tendewa. Katika Kiswahili, dhima ya unufaika inajitokeza katika muundo wa kati wa utendea, kama vile inavyodhihirika katika Kimatengo. Data za Kiswahili zinaonesha kuwa dhima ya unufaika kwa nomino za yambwa tendewa huamuliwa na maana ya msingi ya kitenzi na uhusiano wake na nomino husika za yambwa.

Kwa mfano:

12. (a) Aisha amempikia mgeni chakula.
- (b) Ali atawaletea wageni pombe.
- (c) Ali atawaletea watoto matunda.
- (d) Musa alimtumia baba yake pesa.

**Chanzo:** Khamis (2008)

Nomino ‘mgeni’, ‘wageni’, ‘watoto’ na ‘baba’ katika Data ya 12(a), (b), (c) na (d) mtawalia, ni za yambwa tendewa. Nomino hizo katika sentensi zenye umbo la utendea ni watu wanaonufaika kutokana na vitendo vya ‘kupika chakula’, ‘kuleta pombe’, ‘kuleta matunda’ na ‘kutuma pesa’. Dhima za unufaika zinatokana na maumbo ya utendea zinazoamuliwa na maana ya msingi ya kitenzi na nomino za yambwa pamoja na uhusiano baina vipashio hivyo. Vitenzi vyenye maana tofauti, kama vile ‘nyima’, ‘punguza’ ’iba’ na ‘nyang’anya’ vikitumiwa na nomino za yambwa tendewa hizo (‘chakula’, ‘pombe’, ‘matunda’, na ‘pesa’), vinabadilisha aina ya dhima ya kisemantiki kutoka dhima ya kisemantiki ya unufaika hadi kuwa dhima ya kisemantiki ya uathirika.

### 5.2.2 Dhima ya Uathirika katika Utendea

Uathirika katika taaluma ya isimu ni dhima ya kisemantiki inayotokana na maana ya msingi ya kitenzi na uhusiano wake na yambwa. Dhima hii ya kisemantiki inaweza kudhihirishwa katika maumbo tenda ya vitenzi na katika maumbo nyambuzi ya vitenzi. Dhima ya kisemantiki ya uathirika inaonesha kuwa kishiriki au vishiriki vinaathirika vibaya na matokeo ya kitenzi kilichotumika katika muundo huo. Katika Kimatengo, yambwa tendewa inayozalishwa na umbo la utendea wa kitenzi inaweza kudhihirisha dhima ya kisemantiki ya uathirika. Uwezekano wa udhihirikaji wa dhima ya kisemantiki ya uathirika unaamuliwa na maana msingi ya vitenzi na nomino za Kimatengo kwa pamoja. Katika Data ya 13(a), (b), (c) na (d) imeoneshwa kuwa nomino zote za yambwa tendewa katika sentensi hizo za Kimatengo zinawasilisha washiriki waathirika wa vitendo vinavyotokana na vitenzi ‘juajibila’ (aliwaibia), ‘liahunila’ (aliwatemea), ‘juamisila’ (aliwanyunyizia) na ‘juapojulia huti’ (aliwapiga bunduki).

Kwa mfano:

13. (a) Mwihe juajibila bandu inzeba.  
*Mwizi aliwaibia watu njiwa.*
- (b) Lijoka liahunila abengi imata.  
*Nyoka aliwatemea wawindaji mate.*
- (c) Ndepi juamisila anihenga sumo.  
*Mlevi alimnyunyizia shangazi sumu.*
- (d) Lijambasi liapojulia akapolisi huti.  
*Jambazi aliwafyatulia polisi bunduki.*

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Kwa mujibu wa Data ya 13(a), (b), (c) na (d), maana ya msingi ndiyo inaamua aina ya dhima za kisematiki ya nomino za yambwa. Kutokana na maana ya msingi ya vitenzi vinavyotumika kwenye maumbo ya utendea na uhusiano wake na vishiriki vya ndani kwenye miundo hiyo ya ushiriki, nomino zote za yambwa zinakuwa ni waathirika wa vitendo vinavyofanyika. Katika Kiswahili, vitenzi na yambwa tendewa huchukua nafasi kubwa katika kudhihirisha dhima ya uathirika katika umbo la utendea. Imeshaoneshwa kuwa katika Kimatengo, yambwa tendewa huathiriwa na kitendo au vitendo vinavyotokana na vitenzi nyambuuzi elekezi katika umbo la utendea, hali inayotokea pia katika Kiswahili. Dhima ya uathirika ya kisemantiki inaweza kuonesha kuwa kishiriki au vishiriki katika umbo la ushiriki vimeathiriwa na matokeo ya tendo lililofanywa na kitenzi husika. Data ya 14(a) na (b) inaonesha kwamba dhima ya uathirika kwa yambwa hutumika kuonesha kuwa jambo fulani limefanywa na likamwathiri mtu au kitu kingine. Kwa mfano:

14. (a) Yaya alimlia mtoto chakula.
- (b) Mtoto alimharibia mama kiberiti.

**Chanzo:** Mwita (2014)

Katika Data ya 14(a) na (b), nomino za yambwa tendewa ‘mtoto’ na ‘mama’ katika sentensi hizo zinaonesha vishiriki vimeathiriwa na vitendo vilivyotokana na vitenzi nyambuuzi elekezi ‘alimlia’ na ‘alimharibia’ mtawalia, katika umbo la utendea wa yambwa mbili. Halikadhalika, dhima ya kisemantiki ya uathirika inaamuliwa na maana ya msingi ya vitenzi na yambwa tendewa katika umbo la utendea wa yambwa mbili. Kwa mfano:

15. Wanakijiji walimpigia mwizi kelelele.

**Chanzo:** Matinde (2012)

Katika Data ya 15, yambwa tendewa ‘mwizi’ inaathirika kwa kitendo kinachotokana na vitenzi nyambuuzi ‘walimpigia’. Kama ilivyokwisha kufafanuliwa hapo awali, umbo hili la vitenzi nyambuuzi huweza kusababisha athari kwenye

yambwa tendewa kutokana na maana ya msingi ya vitenzi hivyo na uhusiano wake na nomino hizo za yambwa.

### 5.2.3 Dhima ya Mwelekeo katika Utendea

Dhana ya mwelekeo wa kitendo katika isimu ni dhima ya kisemantiki inayoashiria kuwa kitendo kinachotokea kimeelekezwa kwa mtu au kitu fulani. Katika Kimatengo, kuna vitenzi vichache vinavyoashiria mwelekeo wa kitendo kwenda kwa mshiriki fulani. Baadhi ya vitenzi hivyo ni ‘kanga’ (sukuma), ‘hegakela’ (sogeza), ‘butuka’ (kimbia), ‘lekela’ (tupa), ‘jenda’ (tembea/enda), ‘hatuka’ (harakisha, tembea kwa hatua ndefu), ‘homba’ (ruka) na ‘kelabua’ (rudisha). Nomino za yambwa tendewa zinazotokana na umbo la utendea katika Kimatengo huwa ni mwelekeo wa kitendo wa vitenzi kama hivyo vilivyoorodheshwa kwenye mifano ifuatayo:

Mfano:

16. (a) Atate baahegekeliya ageni uwembi  
*Baba aliwasogezea wageni pombe.*
- (b) Jimbwa jaabutukia abengi  
*Mbwa aliwakimbilia wawindaji.*
- (c) Mwana jwilekelia ingoku ilombi  
*Mtoto aliwatupia kuku mahindi.*
- (d) Nsoko juahombila ambuja bke  
*Mjukuu alimrukia bibi yake.*

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Katika Data ya 16(a), (b), (c) na (d), vitenzi ‘ba-a-hegkel-i-a’ (aliwasogezea), ‘jaabutuk-i-a’ (aliwakimbilia), ‘jwiilekelia’ (aliwatupia) na ‘juahombila’ (alimrukia) vinaonesha mwelekeo kwa nomino za yambwa tendewa ‘ageni’ (wageni), ‘abengi’ (wawindaji), ‘ingoku’ (kuku) na ‘ambuja’(bibi).

### 5.2.4 Dhima ya Kifaa katika Utendea

Umbo la utendea katika lugha za Kibantu linaweza kuzalisha nomino yenye dhima ya kisemantiki ya kifaa cha kutekelezea kitendo (Radford, 2009; Cruse, 2011). Nomino hiyo imeitwa katika utafiti huu kama nomino ya utendea. Uchambuzi na uwasilishaji wa data za utafiti huu katika Kimatengo na Kiswahili umebainisha kwa uwazi aina ya nomino ya utendea. Hii ina maana kuwa nomino utendea ni nomino inayotokea kwenye muundo wa ushiriki wa ndani ambayo inaelezwa kutumika kama chombo cha kutendea kitendo kinachofanyika.

Katika Kimatengo, kuna utokeaji wa nomino ya utendea yenye dhima ya kisemantiki ya chombo cha kutekeleza kitendo fulani. Hata hivyo, data za utafiti huu zinaonesha kuwa kuna vitenzi vichache vinavyoweza kutumika kuzalisha nomino ya utendea katika umbo la utendea yenye dhima ya kisemantiki ya kifaa cha kazi.

Kwa mfano:

17. (a) Abengi bagakomila majani mikoha  
*Wawindaji waliwaua nyani kwa mikuki.*
- (b) Mwanamangongu jualapilia bandu lutela  
*Mwendawazimu aliwapigia watu fimbo.*
- (c) Ndemi juasekulia lijoka ligela  
*Mkulima alikatia nyoka jembe./Alimkata nyoka kwa jembe.*
- (d) Mpisi julikangila linyoto mpeu  
*Mpishi alimsukumia chura fimbo.*

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Katika Data ya 17(a), (b), (c) na (d) nomino ya utendea ‘mikoha’ (mikuki) na ‘lutela’ (fimbo) zinakuwa na dhima ya kisemantiki ya chombo cha kazi. Dhima hiyo ya kisemantiki ya kifaa cha kazi inatokana na maana ya msingi ya vitenzi ‘bagakomila’ (aliwaulia) na ‘jualapulia’ (aliwapigia) ‘juasekulia’ (aliwakatia) na ‘julikangila’ (alisukumia) na uhusiano wake na nomino hizo za utendea. Nomino hizo za utendea zinazuia au kujibu maswali yafuatayo: ‘Aliwaulia nyani kwa kutumia nini?’ ‘Aliwapigia kwa kutumia nini?’ ‘Alimkatia nyoka kwa kutumia nini?’ ‘Alimsukumia chura kwa kutumia nini?’ Kwa maneno mengine ni kwamba, chombo gani kilitumika kutekeleza vitendo hivyo vyote? Aidha, kuna njia mbadala ya dhima ya kisemantiki ya zana ya kazi katika kutekeleza kitendo katika Kimatengo. Njia hiyo ni matumizi ya kihusishi kinachotokea kabla ya nomino za utendea. Data ifuatayo ya 18(a), (b), (c) na (d) imetumika kufafanua hoja hii.

Kwa mfano:

18. (a) Abengi bakoma majani ni mikoha  
*Wawindaji waliua nyani kwa mikuki.*
- (b) Mwnamangongi jualapula bandu nu lutela  
*Mwendawazimu aliwapiga watu kwa fimbo.*
- (c) Ndemi juasekula lijoka ni ligela  
*Mkulima alikata nyoka kwa jembe.*
- (d) Mpisi julikanga linyoto nu mpeu  
*Mpishi alimsukumia chura fimbo.*

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Katika mfano wa Data ya 18(a), (b), (c) na (d), dhima ya semantiki ya zana ya kazi imewasilishwa moja kwa moja na vikundi vihusishi ‘ni mikoha’ (kwa mikuki), ‘nu lutela’ (kwa fimbo), ‘ni ligela’ (kwa jembe) na ‘nu mpeu’ (kwa mkwaju). Nomino hizo zote ni za utendea kwa sababu zinatumika kama vifaa vya kutekelezea kitendo (bakoma), (jualapula), (juasekula) na (julikanga).

Katika Kiswahili, halikadhalika, kuna utokeaji wa nomino ya utendea yenye dhima ya kisemantiki ya chombo cha kutekelezea jambo fulani. Kuna vitenzi vichache katika Kiswahili vinavyoweza kuwa na uelekezi wa umbo la



utendea wenye uwezo wa kuzalisha nomino yenye kuwa na dhima ya kisemantiki ya kifaa. Dhima ya kisemantiki ya kifaa katika Kiswahili huamuliwa na maana ya msingi ya vitenzi na maana ya msingi ya nomino hiyo pamoja na uhusiano wake na nomino ya utendea.

Kwa mfano:

19. (a) Ali ameikatia embe kisu.
- (b) Ali amemfungia kondoo kamba.
- (c) Ali ameukatia muwa panga.
- (d) Ali ameandikia barua unyoya.

**Chanzo:** Khamis (2008)

Katika sentensi hizo za mfano wa Data ya 19(a), (b), (c) na (d) nomino za utendea 'kisu', 'kamba', 'panga', na 'unyoya' mtawalia, zinakuwa na dhima ya kuwa zana ya kutekelezea vitendo kwenye vitenzi 'ameikatia', 'amemfungulia', 'ameukatia' na 'ameandikia'. Katika Kiswahili, kama tulivyoona katika Kimatengo, kuna njia mbadala ya kueleza dhima ya kisemantiki ya kifaa. Njia hiyo mbadala ni matumizi ya vihusishi 'kwa'.

Kwa mfano:

20. (a) Ali amelikata embe kwa kisu.
- (b) Ali amemfungua kondoo kwa kamba.
- (c) Ali ameukata muwa kwa panga.
- (d) Ali ameandika barua kwa unyoya.

**Chanzo:** Khamis (2008)

Katika sentensi za mfano za Data ya 20(a), (b), (c) na (d), uwasilishaji wa dhima ya kisemantiki ya zana ya kutekelezea kitendo umefanywa kwa matumizi ya vikundi vihusishi 'kwa kisu', 'kwa kamba', 'kwa panga' na 'kwa unyoya'. Data ya 20(a), (b), (c) na (d) inaonesha kuwa Kimatengo na Kiswahili zina namna sawa ya kueleza umbo la utendea kuhusiana na dhima ya kifaa ya nomino za utendea.

### 5.2.5 Dhima ya Sababu katika Utendea

Dhima ya sababu ni mojawapo ya dhima za kisemantiki ambapo nomino utendea katika umbo la utendea inawasilisha sababu ya kutekelezwa kwa kitendo. Uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti huu unaonesha kuwa dhima ya sababu ya utekelezaji wa kitendo inajitokeza katika lugha za Kimatengo na Kiswahili halikadhalika. Katika Kimatengo, dhima ya kisemantiki ya sababu kwenye umbo la utendea inawasilishwa kwa Data ya 21(a), (b), (c) na (d). Dhima ya kisemantiki ya sababu ya kitendo inawasilishwa na nomino za utendea ambazo si yambwa kwa sababu hazina sifa za uyambwa.

Kwa mfano:

21. (a) Akatate baalapulia bandu milomo  
*Akina baba waliwapiga watu kwa sababu ya uchokozi.*
- (b) Mpisi juajangatia ageni isima pena  
*Mpishi aliwasaidia watu kwa sababu ya heshima tu.*
- (c) Mbengi juakomila bihe wihe  
*Mwindaji alimwua mwizi kwa sababu ya wizi.*
- (d) Mwenei juakanila bana ikakala  
*Mwenyeji aliwakataa watoto kwa sababu ya uvivu.*

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Data ya 21(a), (b), (c) na (d) inawakilisha dhima ya semantiki ya sababu ya kutekelezwa kwa vitendo. Katika data hizo, nomino tendea ‘milomo’ (uchokozi), ‘isima’ (ukarimu), ‘wihe’ (wizi) na ‘ikakala’ (uvivu) ni vishiriki vya ndani vyenye kubeba dhima ya sababu ya kutekelezwa kwa vitendo. Nomino hizo zote zinawasilisha nomino tendea zinazoonesha sababu ya kitendo kinachotekelezwa. Hata hivyo, nomino hizo tendea si yambwa kwa sababu hazina sifa msingi za yambwa. Katika Kiswahili, dhima ya kisemantiki ya sababu ya kitendo inayotokana na umbo la utendea imewasilishwa kwenye data zifuatazo:

Kwa mfano:

22. (a) Ali amemtumbukizia woga samaki kisimani.  
(b) Bambose amemnyweshea farasi maji huruma.  
(c) Ali alimvalishia Saidi mbwa nguo wazimu.

**Chanzo:** Khamis (2008)

Katika Data ya 22(a), (b) na (c), nomino ‘woga’, ‘huruma’ na ‘wazimu’ ni nomino tendea zinazoonesha sababu ya kitendo kinachotekelezwa. Nomino hizo za utendea zinawasilisha dhima ya kisemantiki ya sababu ya kitendo kwenye umbo la utendea katika Kiswahili. Nomino hizo za utendea si yambwa kwa sababu hazina sifa msingi za yambwa. Kwa hiyo, ingawa kuna vitenzi vichache vinavyoweza kuingia katika umbo tendea, Data za (21) na (22) zinaonesha kuwa lugha za Kimatengo na Kiswahili zinafanana katika uzalishaji wa dhima ya kisemantiki ya sababu ya kitendo.

## 6.0 Hitimisho

Makala hii imechunguza na kufafanua mazingira ya utokeaji wa nomino za yambwa yanayoamuliwa na muundo kati zalishi elekezi wa utendea katika sintaksia ya Kimatengo na Kiswahili. Aidha, imechambua na kufafanua dhima za kisintaksia na kisemantiki za yambwa zinazotokana na muundo kati zalishi wa utendea katika lugha hizo mbili. Muundo zalishi wa utendea unaamua utokeaji wa nomino moja hadi mbili za yambwa. Nomino za yambwa zinazozalishwa na muundo wa utendea katika Kimatengo na Kiswahili ni yambwa tendewa na tendwa. Katika mazingira hayo ya uelekezi wa yambwa mbili, yambwa tendewa

kisintaksia, huitangulia yambwa tendwa kwa sababu nomino ya mtendewa hupewa zaidi uzito wa kisemantiki katika muundo wa sentensi tendea. Kwa ujumla, makala hii imeonesha kuwa mazingira zinamojitokeza yambwa katika lugha ya Kimatengo na Kiswahili yanategemea muundo wa kitenzi. Jambo lingine la kiisimu lililofafanuliwa katika makala hii ni kwamba dhima za kisintaksia na kisemantiki za yambwa tendewa na tendwa zinaamuliwa na maana msingi ya kitenzi husika na nomino zinazokikamilisha kitenzi hicho. Nomino ya yambwa katika muundo wa utendea katika lugha ya Kimatengo na Kiswahili inaweza kuwa na dhima za kisemantiki za unufaika, uathirika, uelekeo, kifaa na sababu. Makala hii inapendekeza kufanyika kwa utafiti zaidi katika lugha za Kibantu ili kufafanua sintaksia na dhima za yambwa kwenye miundo mbalimbali ya vitenzi vya lugha hizo.

### Marejeleo

- Assumpta, K. na Matei, M.A. (2008). *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi Kamili wa Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Barwani, S.S. (1995). *Masomo ya Bidii: A Swahili Intensive Course*. Hamburg: Helmut Buske.
- Besha, R.M. (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: DUP.
- Bresnan, J. na Moshi, L. (1990). "Object Asymmetries in Comparative Bantu." Katika Mchombo, A. (Mh.), *Theoretical Aspect of Bantu Grammar*. Stanford: CSLI Publication.
- Bryman, A. (2004). *Social Research Methods* (Tol. 2). Oxford: Oxford University Press.
- Freeborn, D. (1995). *A Course Book in English Grammar: Standard English and the Dialect* (Tol. 2). London: McMillian Press Ltd.
- Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Msingi wa Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Hyman, L.M. na Duranti, A. (1982). "On the Object Relation in Bantu". *Studies in Transitivity*. 15: 217 – 239.
- Jerono, P. (2003). *Kishazi Huru Arifu cha Kiswahili: Mtazamo wa X-BAA*. Nairobi: University of Nairobi Library.
- Johnson, K. (2004). *Introduction to Transformational Grammar*. Amherst: University of Massachusetts.
- Kapinga, M.C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Khamis, A.M. (2008). *Maendeleo ya Uhusika*. Dar es Salaam: TUKI.
- Kiango, J.G. (2000). *Bantu Lexicography*. Tokyo: ILCAA.
- Kihore, Y.M. (2009). *Stadi za Lugha ya Kiswahili: Sarufi 2*. Dar es Salaam: TUKI.
- Kihore, Y.M. Massamba, D.P.B. na Msanjila, Y.P. (2008). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu Sekondari na Vyuvo*. Dar es Salaam: TUKI.
- Lusekelo, A. (2013). *A Coursebook of Syntactic Theories*. Iringa: Kasenyenda.

- Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M. na Hokororo, J.I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.
- Matinde, R.S. (2012). *Dafina ya Lugha: Isimu na Nadharia*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) LTD.
- Mbele, J. (1999). *Matengo Folktales*. Haverford: Infinity Publishing.
- Mgullu, R.S. (1999). *Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers LTD.
- Mohamed, M.A. (2001). *Modern Swahili Grammar*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mohamed, M.A. (1986). *Sarufi Mpya*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
- Mtesigwa, P.C.K. (2023). Nafasi ya Kiswahili katika Maendeleo ya Viwanda. Katika S. Omari na A. Buberwa (Wah.), *Kiswahili katika Nyanja za Kimataifa*. Dar es Salaam: TUKI.
- Nchimbi, F. (2004). Locative Expressions in Samatengo. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Philipo, Z.T. (2017). *Miundo Msingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Karljamer Publisher Limited.
- Radford, A. (2009). *English Sentence Structure*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Riedel, K. (2009). *The Syntax of Object Marking in Sambia: A Comparative Bantu Perspective*. Netherlands Graduate School of Linguistics: LOT.
- Robins, R.H. (1965). *General Linguistics: An Introductory Survey*. Indiana: Indiana University Press.
- Roy-Campbell, Z.M. na Qorro, M.A.S. (1997). *Language Crisis in Tanzania: The Myth of English Versus Education*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- Rubanza, Y.I. (2003). *Sarufi: Mtazamo wa Kimuundo*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Rugemarila, J.M. (1993). *Runyambo Verbal Extensions and Constraints on Predicate Structure*. Tasnifu ya Uzamivu. Chuo Kikuu cha California.
- Schadeberg, T. (1995). *Aina za Yambwa na Maana Zake*. Leiden: Chuo Kikuu cha Leiden.
- Simango, S. (1995). *The Syntax of Bantu Double Object Constructions*. Tasnifu ya Uzamivu. Chuo Kikuu cha South Carolina.
- Tallerman, M. (2011). *Understanding Syntax* (Tol. 3). London: Hodder Arnold.
- Yule, G. (1985). *The Study of Language*. Cambridge: Cambridge University Press.